**MKOA WA KUSINI**

**WILAYA YA MUHANGA**

| |
|---|
| **KISWAHILI**<br>**Tarehe: 19/Machi/2026**<br>**Wakati: 8h30’-11h30’** |

**MTIHANI WA MWISHO WA WA MUHULA WA PILI**

**KIWANGO: Kidato cha nne**

**MCHEPUO : Lugha**

**MUDA: Masaa matatu (3)**

**ALAMA:** ............./100 **Camis:** .........../70

**MAELEKEZO**

- **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
- **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu tano**
  - . ufahamu ( alama 30),
  - . sarufi na matumizi ya lugha (alama 30),
  - .fasihi (alama 15)
  - . ufupisho ( alama 10)
  - . utungaji ( alama 15)
- **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa**
- **Tumia kalamu ya bluu au nyeusi**

**SEHEMU YA I : UFAHAMU NA MSAMIATI ( Alama 30)**

**Soma kifungu cha habari kinachofuata ,kisha jibu maswali yliyoulizwa juu yake**

**AJALI HAINA KINGA**

"Ajali haina kinga wala kafara." Hivi ndivyo wahenga walivyosema. Na hivi wanakusudia ajali kama vile mafuriko ya mito, moto kuzama kwa merikebu, kuanguka au kulipuka kwa ndege. lakini ajali nyingi nyingine zinakingika iwapo watu watakuwa na hadhari ya kutosha.

Dereva anapopeleka gari kwa kasi hata asiweze kutamalaki usukani, huwa anataraji nini? Au mwendeshaji anapolewa ndi hata gari likawa linayumbayumba huwa amedhamiria kitu gani? Au mpelekaji gari anapotaka kusimamisha gari pindi taa nyekundu inapowaka kwa kuwa eti ana haraka, huwa ameamua jambo gani? Na wale wanaokwenda kwa miguu wanapovuka barabara kwa maringo kama tausi huwa wanamaanisha nini?

Siku hiyo, mvua ilikuwa ikinyesha kwa nguvu sana huku giza limetanda. Ghafula kukasikika "porr!" sauti ya breki ya matatu.Mtoto asiyefisha miaka mitano akaonekana ameanguka mbele ya matatu hiyo.Dereva akitafutwa hayuko,amekimbilia kuinusuru roho yake.Makelele,mayowe na vilio vilisikika hata na viziwi.Wanawake wengine walikuwa wakiragaraga juu ya barabara ilhali wengine walikuwa wakimlaani na kumwapiza dereva."ameshamuua mtoto wetu, damu yake ni halali yetu."Mwanamke mmoja alisema kwa ghadhabu.

"Kila siku ni balaa na beluwa na madereva hawa dawamu wanatutia katika dhiki ambazo hatukuzilalia wala hatukuziamkia," mama mwengine alifoka.Akina mama wengine walishikwa na butaa na bumbuazi

kumuuona mtoto amenyoka na kutulia tuli kama maji ya mtungini.Papo hapo mama mzazi akazirai na akaanguka pu!Walioshuhudia wakaanza kupukutika machozi kupu kupu!

Wema, mwenye duka la samaki hakufadhaishwa na yote hayo kwani alijua wajibu wake ni nini.Akisaidiwa na msamaria mwema,alimchukua mtoto na mama yake na kuwaweka dukani mwake.Akawapa huduma ya kwanza huku mwenziwe akiwapigia simu polisi ambulensi.Fazaa na wahaka ilipotulia watu

walishangaa kuona kwamba mtoto yule alipujuta na kuchubuka tu.Swali wanalojiuliza watu ni kwamba ajali ile ilitokea vipi ilhali mtoto yule alikuwa ameshikwa mkono na mamake?

**Maswali ya ufahamu**

**1.**Kwa kufuatana na taarifa hii ajali inayokingika ni ile ya **( alama2)**

a) Moto. C) Ndege
b) **Barabarani.** C) Majahazi

2.Kati ya watu wane aliowaeleza mwandishi kuwa husababisha ajali,ni yupi hatari Zaidi**?(Alama 2)**

a) Mpelekaji kwa kasi c) Avukaye barabara taratibu
b) Mpelekaji mlevi **d) Dereva asiyetambua taa nyekundu.**

3.Dereva alikimbia kwa kuwa................
**( Alama2**)

a) Hana cheti cha kupeleka gari. C)Gari halikuweza kuenda
b) **Alikuwa ameshagonga mtoto.** D)Alihofia kuuliwa.

4.”Damu yake ni hatali yetu”walikusudia
**(Aama2)**

a) Kumsaidia kwa kumpa damu. D) Kutokubali kula chake.
b) **Kumuua** d) Kula mnyama atakayempika kam sadaka.

5.Kinyume cha mayowe ni
**(Alama2)**

a) Makelele c) Mshangao
b) **Vigelegele** d) Furaha

6. Kwa nini akina mama wengine walishikwa na butaa na bumbuazi? **( Alama2**)

**Akina mama wengine walishikwa na butaa na bumbuazi kwa sababu walimuona mtoto akinyooka na kutulia tuli kama maji mtungini. Akina mama hawa walimuonea huruma mtoto huyo kisha wakashikwa na butaa.**

7. Papo hapo mama mzazi akazirai na akaanguka pu! “pu” maneno kama hili ya kuiga na kunakili milio ya sauti huitwaje katika Kiswahili? **(Alama2)**

…… **tanakali sauti**

8. Je ni kweli kwamba ajali haina kinga? Eleza ! **(Alama2)**

**Ndiyo, ajali haina kinga wala kafara kama kifungu hiki kisemacho**

9. Fafanua kwa nini mwenye duka hakufadhaishwa na yote hapo? (**Alama2)**

.. **Mwenye duka hakufadhaishwa na yote hapo kwa sababu alijua wajibu wake, alichukua mtoto na mama yake na kuwaweka dukani mwake. Akawapa huduma ya kwanza huku mwenziwe akiwapigia simu polisi na ambulensi**

10. Unafikiri mwenziwe ni nani aliyekuwa akiwapigia simu polisi na ambulensi. **( Alama2 )**

**Kama walivyotuambia kwamba alisaidiwa na msamaria mwema, huyu msamaria mwema ndiye mwenziwe**.

**11**. Eleza maana ya maneno haya na uyatumie kutoka kifungu cha habari ulichopewa kuunda sentensi yeenye maana **.( Alama10)**

a) Hadhari……… **uangalifu, tahadhari**

b) Kutamalaki… **kuwa na mamlaka ya kitu fulani; kumiliki; kutawala.**

c) Kuyumbayumba………… **kuhangaika; kwenda huku na huku kama vile mti mrefu unaopigwa na upepo**

d) Kugaragara…… **kugeukageuka mahali ulipolala.**

e) Kupukutika… **kudondoka kwa majani kutoka kwenye mti**

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama30)**

**12. (Alama 10)**

| |
|---|
| Kutendekeza,bilakiasi,alizirai,kutamalaki,kama tausi,kuwaapiza,alirukaruka,lililipuka, limedhamiria,butaa,furaha,samani. |

1. Bomu **lilipuka.**na watu wengi wakapoteza maisha yao.
2. Ni umuhimu kwetu…**kutamalaki**….nafsi zetu tunapoona ajali.
3. …**Samani**.za nyumba yangu zilitengenezwa na seremala wanchi ya ng'ambo.
4. Mwanafunzi…**alizirai** alipoambiwa ameanguka mtihani.
5. Jangili hili **limedhamiria** .mabaya ndipo likaingia nyumbani na kisu mkononi.
6. ……**Aligaaga..**juu ya ardhi alipofahamishwa kwamba mzazi wake amefariki baharini.
7. Maradhi haya ameyapata kwa kupenda kula..**bila kiasi**
8. Bibi harusi alipanda jukwaa kwa maringo…**kama tausi**
9. Alipigwa na…**butaa..** alipoona amepoteza pesa zake zote katika gari.
10. Ni makosa kwa wazazi…**kutendekeza**….watoto wao wanapowakosea.

**13. Badilisha sentensi zifuatazo katika hali yakinishi au kanushi ( Alama 5)**

1. Mwizi amekamatwa.

………**hajakamatwa**

2. Msingekuwa hodari, pesa zenu zingemalizika.

… **Mngekuwa**……..**zisingemalizika**

3. Heshimu muda unaopewa.

……… **usiheshimu…**

4. Sikio la kufa halina dawa.

…………**lina** dawa

5. Tutaenda mjini pamoja naye.

………**hatutaenda**

**14. Tumia vivumishi viulizi ambavyo ulipewa ndani ya mabano kujaza sentensi. (Alama 5)**

1. Jibu .....**lipi**......... limeishapatikana? (-pi)

2. Mawe ..**mangapi**... yamewekwa kando ya barabara. (-ngapi)

3.Madirisha ..**gani**......... yamefunguliwa. (gani)

4. Meno **.....yapi..........** yameng'oka. (-pi)

5.Tunda **.........gani......** limeiva. (gani)

**15. Tumia '-ote-' au 'o-ote' pamoja na viambishi sahihi vya ngeli kujazia pengo katika sentensi zifuatazo.( Alama 5)**

1. Nitatumia jembe.........**lolote**...................nitakalopewa.

2. Mihogo.....................**yote**.............imevunwa.

3. Kuku ...............**wote**.................wamepewa chakula.

4. Sitachukua nanasi ...**lolote**.....................................

5. Fyeka nyasi nyasi......**zote............................**

**16. Sahihisha makosa yanayopatikana ndani mwa sentensi hizi.** (**Alama 5**)

1.Sipendi kutembea mahali mabaya yasipo na mazingira bora.

...... **Pa**baya **pa**sipo

2. Kijana kipi ni mzuri?

......**yu**pi

3. Mwanafunzi mdohari hufanikiwa.

............**hodar**i

4.Zawadi kirefu anatembea polepole.

.........**mrefu**

5. Wakiristo anampenda kumsifu Mungu.

............**wanapenda**...

**SEHEMU YA III: FASIHI** **( Alama 15)**

**17.** Sanaa ni nini**?** **(Alama 2)**

**... Sanaa ni ufundi wa kuwakilisha mawazo na hisia alizonazo binadamu kwa njia ya ubunifu.**

**18. Jaza methali zifuatazo (alama 3)**

**a)** Chombo cha kuzama ,**hakina usukani**……

b) **Ngoja ngoja**……..,yaumiza matumbo

c) Asiyefunzwa na mamaye, **hufunzwa na ulimwengu**……….

**19. Tumia mshale kuoanisha nahau au misemo ifuatayo kutoka sehemu A na maana zake kutoka sehemu B (Alama 10)**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| a.Kupiga mali shoka | 1.Kutokuwa na matumaini tena |
| b.Kumezea mate | 2.Kuwa na maneno makali |
| c.Kukata tamaa | 3.Kupata mateso makali |
| d.Kuwa na ulimi wa upanga | 4.Kugawana mali |
| e.Kuona/ kupata cha mtema kuni | 5.Kutamani sana |

**A → 4**

**B → 5**

**C →1**

**D →2**

**E →3**

**SEHEMU YA IV: UFUPISHO ( Alama 10)**

**20. Kwa kuzingatia kanuni na sifa za muhtasari ,fupisha kifungu cha habari kifuatacho:**

**Sungura na Mamba**

Hapo zamani mamba alikuwa na meno mazuri sana. Wanyama wengi waliyapenda meno yake. Baadhi yao walisikia wakitia chumvi kuwa meno ya mamba yalikuwa na thamani sawa na dhahabu.

Mamba huyo alipotangaza nia yake ya kujipatia jiko karibu kila mnyama aliyekuwa na binti mzuri alitaka binti yake aolewe naye. Hivyo mabinti wengi walionekana wakijipitisha mbele ya mamba huku mmoja akiwa amejipamba vizuri ili kuweza kuliteka penzi lake.

Hali hiyo haikumpendeza kabisa Sungura. Kwani miongoni mwa hao wasichana waliojitokeza, alikuwepo mmoja aliyependwa sana na Sungura. Hivyo, Sungura wakati wote alikuwa akiwaza la kufanya ili kumwangusha Mamba.

Siku moja Sungura alipita nyumbani kwa Mamba, na kumkuta amelala fofofo chini ya kivuli cha mti huku meno yake mazuri yakionekana waziwazi. Hapo Sungura aliweza kuyaona maganda mengi ya karanga na akagundua kuwa Mamba alikuwa akitafuna karanga.

Siku nyingine Sungura alikuja tena nyumbani kwa Mamba. Akamwambia, “Rafiki yangu nimekuchukulia zawadi nzuri uipendayo.”Zawadi gani?” “karanga”, alijibu Sungura huku akimwonyesha mamba mfuko uliojaa karanga.

Mamba alipouona mfuko huo, aliurukia mfuko akaliingiza domo lake refu ndani na kuanza kutafuna kwa pupa. “Mama wee !” Mamba alisikika akilia huku mikono yake akishikilia mdomo wake ambao sasa umejaa damu. Meno yake mengi yaling’oka pia. Kumbe ndani ya mfuko ule Sungura aliweka mawe mengi na njugu nyasa chache tu. Mamba alipojaribu kutafuna alichofikiria kuwa ni karanga, meno yake mengi yaling’oka.

Sungura alipoona mbinu yake imefaulu, aliondoka na kuelekea kwake kwa furaha. Siku hiyo jioni, wanyama wengi walishangaa kumuona Sungura alikuwa amevaa miwani na kupepesuka ovyo. Kumbe alikuwa akisherekea ushindi wake dhidi ya mamba.

Habari za Mamba kung’olewa meno yake zilienea kwa haraka sana. Wasichana wote walipopata habari hizo, walibadilisha mawazo yao ya kutaka kuolewa na Mamba ambaye sasa alikuwa kibogoyo na kuchukiza sana.

**MWONGOZO WA KUTOA UFUPISHO**

1. **Kichwa (alama1)**

2. **Urefu (alama 2)**
3. **Pembezo (alama 2)**
4. **Usafi (alama 2)**
5. **Sarufi na matumizi ya lugha (alma 3)**

**SEHEMU YA V: UTUNGAJI (Alama 15)**

21. Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge insha yenye maneno kati ya 150 na 200.

a) " Lugha ndio uti wa mgongo wa utamaduni " Eleza

b) Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

**Mwongozo wa kukosoa insha**

**FANI**

-Kichwa/Mada **(alama 2)**

- Urefu wa insha **( alama 1)**

-Pembezo: **(alama 1)**

-Usafi **( alama 1)**

**MAUDHUI**

- Utangulizi: **( alama 1)**
- Mwili: maelezo ya hoja angalau tatu (alama 7): Sarufi na matumizi ya lugha **(alama1)**
  ( makossa mawili ni kutoa alama 0.5;makossa manne ni kutoa alama 1)
- Hitimisho **( alama2**)

**-Mwisho-**